**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

Mkuu wa Shule: 0755-148 420/0629116787

Makamu Mkuu wa Shule: 0752-554 064

Patron: 0769-488 300

Shule ya Sekondari VUMA,

S.L.P 718,

**SUMBAWANGA.**

**17/04/2024.**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..........................................................................

S.L.P ...............................

.......................................................................

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI VUMA HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA MKOA RUKWA MWAKA 2024**

1 . Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidało cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya..........

Shule ya Sekondari Vuma ipo umbali wa Kilometa 85 Kaskazini Mashariki mwa Mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Sumbawanga mjini. Nauli ni Shilingi **8,000/=** kwa basi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **30/06/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/07/2024**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali moja nyeusi na suruali moja rangi ya bluu bahari.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo ni track suit ya bluu 1, bukta 1 rangi ya bluu na raba rangi yoyote
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
v. Soksi jozi mbili nyeusi
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
vii. Sweta moja dark blue yenye shingo ya V
viii. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali ya khaki na T- Shirt ya bluu
ix. Tai nyeusi moja na bluu bahari moja.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa (Counter book Q4) saba
ii. Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo futi mbili na nusu
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu na chandarua
vi. Nguo za ndani za kutosha
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 . | Mchango wa Uendesha•i wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii ilipwe kwenye Akaunti Na. 62110031123 - VI-WIA SELF RELIANCE Benki ya NMB na mwanafunzi aje na hati ya malipo (pay in slip)**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais — TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kvva maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
vi. Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
ix. Uvutaji wa sigara
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kusababisha mimba, xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xv. Kudharau Bendera ya Taifa
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule: ........................................

Jina la Mkuu wa Shule: **THOMAS NICHOLAUS**

THE HEADMASTER
VUMA SEC. SCHOOL
Mhuri wa Mkuu wa Shule: S'WANGA........................................

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

> Mkuu wa shule: 0755-148 420/0629116787
> Makamu Mkuu wa Shule: 0752-554 064
> Mwandamizi Taaluma: 0756-716 031
> Mwandamizi Malezi: 0769-488 300







**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

VUMA SEC. SCHOOL

P.O BOX 718

**SUMBAWANGA**

DATE: ………………….

MEDICAL OFFICER

GOVERNMENT HOSPITAL

……………………………………….

**REF. REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

NAME OF STUDENT: ……………………………………………………………………………

Please examine the above named as to his fitness as indicated below and for necessary treatment if required.

This certificate must be signed by a qualified medical officer of a government hospital and returned to school by student.

**MEDICAL CERTIFICATE**

Skin ……………………………………………………………………… Abdomen ……………………………………………………………………

Eyes ……………………………………………………………………… Stool …………………………………………………………………………

Ears ……………………………………………………………………… Urine …………………………………………………………………………

Teeth …………………………………………………………………… H.B Haemoglobin …………………………………………………

Spleen …………………………………………………………………… Chest …………………………………………………………………………

Any disability ………………………………………………………………………………………………………………………………………………

I consider that:

1. He is in good health, free from infection diseases, worms, bithasia and is fit to come to school
2. He is fit to come to school after having ……………………………………………………………… Treatment

………………………………………………… ……………………………

MEDICAL OFICER DATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI VUMA**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VUMA**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. JINA LANGU ....................................................................................................................
2. SHULE YA MSINGI NILIYOSOMA INAITWA ......................................................................
3. UMRI WANGU NI MIAKA ................................ NIMEZALIWA TAREHE ................................
4. KIMO KATIKA SENTIMITA ......................................
5. JINA KAMILI LA BABA YANGU MZAZI NI ..........................................................................
6. JINA KAMILI LA MAMA YANGU MZAZI NI .........................................................................
7. NILIZALIWA (MAHALI) ............................................................ (WILAYA) ............................
8. KABILA LANGU NI .............................................. WA MKOA WA .........................................
9. NIMEKUJA KUSOMA SHULE YA SEKONDARI VUMA;
   a) NIMECHAGULIWA/NIMEHAMIA ..................................................................
10. KWA KUWA NIMEKUBALI NA NIMEIHARI KUSOMA SHULE YA SEKONDARI VUMA, IFUATAYO HAPO CHINI NI AHADI YANGU YA MKATABA NA MKUU WA SHULE KWAMBA:-
    a) NITAKUWA MTIIFU WA SHERIA ZA SHULE ZOTE PAMOJA NA UONGOZI WA SHULE KUANZIA NGAZI YA KIONGOZI MWANAFUNZI DARASANI.
    b) NITAKUWA MSTARI WA MBELE KWA KUSHIRIKI KAZI ZOTE ZA SHULE, MASOMO, MICHEZO, USAFI NA UZALISHAI MALI
    c) NITAKUWA MFANO MWEMA KATIKA TABIA NA MWENENDO, NIKIWA NDANI NA NJE YA MIPAKA YA SHULE KWA MANUFAA YANGU KITAALUMA NA MAADILI PIA KWA HESHIMA YA WAZAZI, WALIMU, SHULE, WILAYA, MKOA NA TAIFA
    d) SINTASHIRIKI KWENYE MGOMO WA AINA YOYOTE AU KUSHAWISHI MGOMO. NITAFUATA KANUNI NA TARATIBU PALE NINAPOKUWA SIJUI JAMBO KWA KWENDA KULIZA KATIKA OFISI YA MKUU WA SHULE YA WALIMU KUPEWA UFAFANUZI ZAIDI.
    e) SAHIHI YA MWANAFUNZI: ...................................................................................... TAHERE: ..............................................

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

1. JINA LA MZAZI/MLEZI .......................................................................................................
2. UNAPOKAA KWA SASA (KIJIJI/MJI) .......................................................................................
3. ANWANI ...........................................................................................................................
4. KAZI .................................................................................................................................
5. DINI .................................................................................................................................
6. UHUSIANO NA MWANAFUNZI ..........................................................................................
7. MZALIWA WA MKOA ..................................... WILAYA ...................................................
8. KWA KUWA NAHAKIKISHA MWANAFUNZI ALIYETAJWA HAPO JUU, ATAJIUNGA NA KUSOMA SHULE YA SEKONDARI VUMA MPAKA KUHITIMU KIDATO CHA SITA, NAAHIDI KWAMBA:-
   a) NITAMPATIA MAHITAJI YOTE YANAYOTAKIWA ILI AWEZE KUSOMA
   b) NITAMHIMIZA KUWA NA MAHUDHURIO MAZURI YA SHULE KILA SIKU
   c) NITASHIRIKIANA NA UONGOZI WA SHULE KATIKA KUMPATIA MALEZI BORA/MAADILI MPAKA ATAKAPO MALIZA MASOMO YAKE
   d) KUTOKEAPO TATIZO, NITAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KWA MAANDISHI AU KUFIKA MIMI MWENYEWE OFISINI

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI...................................................................................... TAREHE ..........................................